**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 24/12/2021 KUJADILI TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI NOVEMBA**

**MAHUDHURIO:**

**Wajumbe:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mh. Desderius O.Haule | Mwenyekiti | |
| 2. Ndugu Juma H. Juma | Mkurugenzi Mtendaji | Katibu |
| 3. Mh. Bahati G. Mbele | Makamu Mwenyekiti | |
| 4. Mh. Bosco Kapela | Mjumbe | |
| 5. Mh. Evelin Mwitumba | Mjumbe | |
| 6. Mh. Bosco Ndimbo | Mjumbe | |
| 7. Mh. Upendo Komba | Mjumbe | |
| 8. Mh. Gaudensia Kapinga | Mjumbe | |
| 9. Mh. Rehema Ndunguru | Mjumbe | |
| 10. Mh. Aron Hyera | Mjumbe | |
| 11. Mh. Bruno Kapinga | Mjumbe | |

**Wasiohudhuria:**

1. Mh. Benaya L.Kapinga (Mbunge) Mjumbe – kwa taarifa

**WATAALAM**

| | |
|---|---|
| 1. Ndugu Stephen Mapunda | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utumishi |
| 2. Ndugu Paschal Ndunguru | Mkuu wa idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 3. Ndugu Hillary Joseph | Kaimu Mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 4. Eng. Neema Mbilinyi | Kaimu mkuu wa idara ya Ujenzi |
| 5. Ndugu Sarah Komba | Kaim Mkuu wa Idara ya Afya |
| 6. Ndugu Sylivia Mlelwa | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 7. Dr. Patrick P.Banzi | Mkuu wa Idara ya Mifugo |
| 8. Ndugu Jobu Mwalukosya | Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 9. Ndugu Asante Luambano | Mratibu wa TASAF |
| 10. Ndugu Sosteness Nakamo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mazingira |
| 11. Eng. Evance Haule | Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika |
| 12. Ndugu John Kabada | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 13. Ndugu Salum Said | Kaimu Mkuu wa kitengo cha Nyuki |
| 14. Ndugu Rogatus Mapunda | Mthibiti Ubora wa Shule |
| 15. Ndugu Maurus B. Hyera | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili |
| 16. Ndugu Flavian Nombo | Kaimu Mweka Hazina |
| 17. Ndugu Venant Kumburu | Afisa Utumishi |
| 18. Ndugu Grace Mbena | Katibu TSC |
| 19. Ndugu Hussein Khanga | Afisa Utamaduni |
| 20. Ndugu Andrew Mbunda | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 21. Ndugu Peter Ntalamuka | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 22. Ndugu Pisii Nassoro | Afisa Uvuvi |

**AGENDA**

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa tarehe 26.11.2021
4. Yatokanayo na muhtasari huo
5. Taarifa ya mapato na matumizi Mwezi Novemba 2021
6. Taarifa ya Mapokezi fedha Tshs 590,000,000 kwa ajili ya miundombinu ya Afya
7. Taarifa ya Usajili na Utambuzi wa Mifugo
8. Mengineyo
9. Kufunga kikao

**MDC/FUM/46/2021-2022: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 04:11 Asubuhi kwa kuwashukuru wakuu wa Idara kuandaa vizuri taarifa.

**MDC/ FUM /47/2021-2022: KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zilisomwa na kupokelewa na wajumbe.

**MDC/ FUM /48/2021-2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA TAREHE 26.11.2021**

Muhtasari huo ulisomwa kisha ulipitiwa na wajumbe kwa ajili ya kufanya marekebisho ya uandishi kisha ulithibitishwa kuwa ni kumbukumbu ya Halmashauri

**MDC/ FUM /49/2021-2022:YATOKANAYO NA MUHTASARI HUO**

**Ifuatiliwe taarifa sahihi za idadi za Kilo za kahawa zilizouzwa**. Taarifa iliandaliwa na kuwasilishwa kwenye kikao.

Taarifa hiyo baada ya kuwasilishwa wajumbe waliazimia yafuatayo :-

-Kufuatia ushuru wa kahawa tani 9 toka AMCOS ya Lukarasi

-Vyama vya Ushirika vikaguliwe ili kupata taarifa za fedha za chama na ushuru wa Halmashauri

**MDC/FUM/50/2021-2022: KUJADILI TAARIFA YA FEDHA (MAPATO NA MATUMIZI) YA MWEZI NOVEMBA 2021**

Kaimu Mweka Hazina wa Halmashauri aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi Novemba 2021, katika taarifa yake alieleza kuwa Halmashauri imekusanya fedha Tshs bil. 1.4 kati ya Bil. 1.9 zilizotakiwa kukusanywa kwa kipindi cha miezi mitano.

Kwa upande wa vyanzo fungwa alisema, Halmashauri imekusanya Tshs Mil. 346,412,410 kati ya Tshs Mil. 284,120,000 sawa na asilimia 122% ya lengo la miezi 5. Aidha alisema kufikia Novemba wastani wa makusanyo kwa miezi mitano ni asilimia 51% ya makisio ya mwaka mzima sawa na kiasi cha Fedha Tsh Mil. 681,888,000.

Pia alielezea mapato yatokanayo na ruzuku mbalimbali ambapo alisema,
-Mishahara, kiasi kilichopokelewa ni Tsh bil.8.7 kati ya Tshs bil. 8.9

-Ruzuku ya matumizi mengineyo, kiasi kilichopokelewa ni Tshs bil. 1.4 kati ya mil. 842,938,313.75 sawa na 168%.

-Ruzuku ya miradi, kiasi kilichopokelewa kwa ajili ya miradi ya Maendeleo ni Tshs bil.3.1 kati ya bil. 3.9 sawa na 79% ya fedha zilizotarajiwa kupokelewa.

-Elimu bure alisema Halmashauri imepokea Mil. 690,307,855 ikiwa sawa na 39% ya makisio ya mwaka ambayo sawa na jumla ya Tshs Bil. 1.8 kwa mwaka mzima.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:-
Akichangia Mheshimiwa Diwani wa Lukarasi Bosco Ndimbo alipenda kujua maendeleo ya kaya mpya zilizoibuliwa kwa ajili ya kunufaika na TASAF.
Akijibia suala hilo Mratibu wa TASAF alisema, walengwa hao wataanza kulipwa fedha zao kuanzia awamu inayokuja.

**MDC/FUM/51/2021-2022 : TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA TSHS 590,000,000 KWA AJILI YA MIUNDOMBINU YA AFYA**

Akiwasilisha taarifa hiyo Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya alisema, Halmasahuri imepokea Jumla ya Tshs Mil. 590 kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya miundombinu ya Afya kwa zahanati ya Kindimba Chini sh Mil. 250, Ujenzi wa Nyumba ya Mtumishi Tshs Mil. 90 na Ujenzi wa jengo la wagonjwa mahututi ni mil. 250.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo :-

Akichangia Mheshimiwa Diwani wa Lukarasi Bosco Ndimbo alishukuru kwa mapokezi ya fedha hizo.

Akichangia Diwani wa Kata ya Ukata alishukuru kwa mapokezi ya Fedha hizo na kumwomba katibu aone uwezekano wa kuwasaidia kata ya Namswea ili kuwapa bati ili ziwasaidie kuezeka jengo ambalo limeshapauliwa kwa nguvu za wananchi.

Akifafanua Katibu alisema , miradi yote inayotekelezwa ni lazima iwekwe kwenye bajeti ya mwaka husika. Hivyo alishauri jengo hilo liwekwe kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 ili liezekwe.
Akiendelea kuelekeza alisema hata akipewa fedha za kununua bati itakuwa bado jengo husika haliwezi kutoa hauduma hivyo ni lazima liwekwe katika bajeti ili jengo hilo likamilike na kutoa huduma kwa wananchi.

Akiunga hoja Diwani wa Lukarasi Bosco Ndimbo alisema, miradi inayotekelezwa ni lazima iwepo kwenye bajeti.

Akichangia Mwenyekiti alisema yapo maboma mengi huko vijijini yasiyokuwepo kwenye bajeti, hivyo aliwahimiza wajumbe kuwa wananchi watumie nguvu zao ili wakamilishe ujenzi huo.

**MDC/FUM /52/2021-2022 : TAARIFA YA USAJILI, UTAMBUZI NA UFUATILIAJI WA MIFUGO**
Akiwasilisha taarifa hiyo Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi alisema, ili kufanikisha zoezi hilo inahitajika jumla ya Tshs 9,030,000/= .

Akiendelea kufafanua alisema suala hilo ni muhimu sana kwa kuwa lina faida nyingi ikiwemo, uhakika wa soko, kudhibiti wizi wa mifugo, kuwezesha bima na mikopo kwa wafugaji, mifugo kutambuliwa na kukabiliana na magonjwa.
Akielezea kuhusu mifugo inayolengwa katika zoezi hilo alisema ni ;-
-Ng'ombe
-Punda
-Mbuzi na
Kondoo

Akihitimisha alisema utambuzi huo utakuwa kwa njia ya kuweka Hereni kwenye sikio la kila mnyama anayesajiliwa.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuchangia kama ifuatavyo :-

Akichangia Mheshimiwa Diwani wa Mkumbi Ndugu Bruno Kapinga aliwashauri wajumbe kuwaandaa wananchi kwa ajili ya utambuzi huo ili zoezi litakapoanza litekelezwe kwa uraisi.

**MDC/FUM /53/2021-2022 :MENGINEYO**

Akichangia Mheshimiwa wa kata ya Ukata ndugu Evelin Mwitumba aliuliza juu ya huduma ya Bima za Afya kwa madiwani kufuatia usumbufu wanaoupata wanapokwenda Hospitali na wanakosa huduma kwa kutolipia.

Akijibia Katibu alisema Halmashauri itaendelea kulipa 3% ili Waheshimiwa Madiwani waendelee kupata huduma hiyo.

Akichangia Mwenyekiti alisisitiza juu ya sula la bima za madiwani kwa kumwomba Katibu kufuatilia na kupata ufumbuzi.

Akipokea agizo hilo Katibu alisema, atakaa na Kaimu MwekaHazina ili kulipatia ufumbuzi jambo hilo. Mwisho aliwatakia wajumbe wote sikukuu njema ya Krismass na Mwaka mpya 2022.

**MDC/FUM /54/2021-2022:KUFUNGA KIKAO**

Kabla ya kufunga M/kiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na kuwapongeza wakuu wa Idara kwa maandalizi mazuri ya taarifa kasha aliwatakia wajumbe wote mapokezi mema ya sikuku ya Krismass na mwaka Mpya. Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 5:13 asubuhi.

**=UMETHIBITISHWA=**

**MWENYEKITI :**........................ **KATIBU :**........................................

**TAREHE :** 28/1/2022